UBAINIFU YAKINIFU

(kuhusu makosa ya kimanhaji na kielimu, yaliofanywa na baadhi ya wanaojinasibisha na maswala ya elimu)

MAKALA NO (6)

IMEANDIKWA NA:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM

١٤٣٨/٤/١٩هـ

بسم الله الرحمن الرحيم.

الحمد لله رب العالمين، والصلاة والسلام على النبي الكريم، وعلى آله وأصحابه أجمعين.

أما بعد.

Baada ya kumshukuru Allah Mtukufu, na kumswalia Mtume wetu kipenzi, na Ahli zake, na Maswahaba wake wote:

Ndugu msomaji, ni wazi kua tumeelewa vya kutosha, jinsi gani Abdu Rrah'man na Ame, wameingia kwenye makosa makubwa sana, ya kuwatoa watenda madhambi makubwa, kwenye kuingia kwenye walaya ya Allah moja kwa moja!

Na tumeona maneno ya ulamaa, kwa dalili mbali mbali, yakionyesha kua kila muislamu anaingia katika Hizbu Llaah na Mawalii wa Alla, kwa kadri ya Imani yake, na matendo yake, Lakini kwa istilahi maalumu, inapokusudiwa waislamu wamchao Alla na walio shikamana na dini kisawa sawa, basi waislamu watu wa sunna na uchamungu ndio mawalii wa Alla na hizbu yake.

Na wanavyotajwa waislamu kwa ujumla dhidi ya makafiri, basi waislamu wote wanakua Hizbu Llaah, kila mmoja kwa kadri ya imani yake na matendo yake, na makafiri ni Hizbu Sshaitwaan iliyokamilika.

Miongoni mwa maneno ya abdru Rrah'man ya kusisitiza kuwatoa kwake waislamu wa madhambi

makubwa moja kwa moja kwenye Hizbu Llaah na Mawalii wa Alla: amekuja na maneno yafuatayo **kama ninavyo yanukuu neno kwa neno:**

"Kwa sababu ahlussunna wal jamaa'a, wanagawanyisha ri'ayatullaah mauunatullaah alaa qismaini, kwa maana msaada wake Allah na riaya yake Allah tabaaraka wata'ala vinagawanyika sehemu mbili.

Sehemu ya kwanza aaamma, ni kwa ujumla, inaingia kwa watu wote, mubtadia, kaafiri, dhwaalim, faasiq.

Na maana nyingine, ni mauunatullaahi khaassswa, kwa maana inakua msaada wake Allah maalumu kwa watu wake maalumu, ambao haupatikani, illaa alal anbiyaau, wa alaa Rusulih, na juu ya manabii wake na Mitume wake.

na kadhaalika wale ambao wenye kushikamana na sharia zake allah tabaaraka wata'aalaa,Na hii maana ndio iliokusudiwa katika aya hii"

(Rejea sauti ya kalima yake aliyonijibu)

Abdurrah'maan hapo, amesema watu wamegawanyika katika swala la walaya ya Allah na hizbu yake na riaya (uangalizi na msaada) wake makundi mawili:

KUNDI LA KWANZA:

Linaingia watu wote, makafiri watu wa bida'a, mafasiki, na nk.

KUNDI LA PILI:

Linaingia tu watu wema, walioshikamana na dini kikamilifu, kuanzia Manabii, Mitume, Maswahaba, na wengineo,na kua huu ni uangalizi na msaada maalumu ambao haupatikani isipokua kwa watu wema tu wenye imani kamili, wasiokua wafanya madhambi makubwa.

Na akadai kua maana hiyo ya watu maalumu tu waliokamilika imani, ndio iliokusudiwa kwenye Aya ya kuhusu Hizbu Llaah na Hizbu Sshaitwaan.

MAJIBU YETU YENYE UFAFANUZI:

KWANZA:

Umepita ufafanuzi wa kutosha kuhusu matumizi

ya neno Hizbu Llaah na Hizbu Sshaitwaan, ambalo ni sawa na neno Waliyyu Llaah na Waliyyu Sshaitwaan, na tumeona kua neno Hizbu Llaah, na neno Waliyyu Llaah linatumika kwa maana zote mbili, Maana ya kiujumla, na maana maalumu.

Na tumeeleza kua mtiririko wa maudhui ndio unahukumu makusudio ya neno Hizbu Llaah na Waliyyu Llaah, kwani ikiwa itakusudiwa waislamu wote kwa ujumla dhidi ya makafiri, hakika kila muislamu anaingia katika Hizbu Llaah na Waliyyu Llaah, kila mmoja kwa kadri ya Imani yake.

Ama ikiwa mtiririko wa maudhui unakusudia kutofautisha kati ya waislamu wema na waislamu waovu, basi Ahlussunna na wenye kushikamana na twa'a ndio Hizbu Llaah, kwakua wamekamilika imani zao kwa kadri ya uwezo wao, na ndio pekee huitwa Hizbu LLaah na Mawalii wa Allah.

(kwamaana huwezi kuita kundi flani la bida'a au kumuita mtu flani wa bida'a ukasema: yule ni walii wa Alla, kwakua kuwaita watu maalumu kama hivi kunakua kwa maana maalumu tu ambayo ni ya Ahlussunna na uchamungu).

Ama watu wa bida'a na mafasiki: hawa wanakua ni sehemu ya Hizbu Sshaitwaan kwenye bida'a zao, lakini hawatoki kwenye Hizbu Llaah na Mawalii wa Allah kwa maana ya Ujumla.

Na hivyo hao mafasiki au watu wa bida'a wanapoitwa Hizbu Sshaitwaan na Mawalii wa shetani: ni kwenye Mlango wa bida'a zao na maasi yao tu, na hivyo hawawi kwenye Hizbu Sshaitwaan kikamilifu kama walivyo makafiri.

Na tumetoa dalili mbali mbali, katika kitabu kitukufu cha Alla, na ufafanuzi wa maulamaa juu ya hilo.

Na tumeona kua kuwatoa moja kwa moja waislamu wenye madhambi makubwa kwenye walaya ya Allah na Hizbu yake kwa maana ya ujumla, hii ni itikadi ya kikhawariji!

PILI:

Ni kweli kua Ri'aya (uangalizi) wa Alla, umegawanyika sehemu mbili.Lakini je, huu ni mgawanyo wa aina gani?

JAWABU:

Huu ni mgawanyo wa kuangalia watu wote(Waislamu na wasiokua Waislamu), ambapo kwa kuzingatia aina hii uangalizi wa Alla unagawanyika sehemu mbili:

SEHEMU YA KWANZA:

Ni riaya(uangalizi) unaoenea kwa kila kiumbe, awe muumini, au kafiri, nao ni uangalizi wa kuwaruzuku, kuwateza nguvu, kuwapa riziki, na n k. Uangalizi huu anaupata kila mmoja, muislamu na asiyemuislamu.

SEHEMU YA PILI:

Ni riaya(uangalizi) wa Allah ambao ni maalumu kwa waumini (waislamu), nao ni uangalizi wa

kuwaafikisha kwenye haki, na kuwanusuru, na kuwakurubisha kwake.

Na kwa hakika kila muumini, anaingia kwenye uangalizi huu kwa kadri ya imani yake na matendo yake, kwani tumeona katika dalili na ufafanuzi wa wanachuoni:

Kua wanapotajwa waumini na mawalii wa Alla kwa maana ya ujumla huingia kila mwenye chembe ya Imani, kwani muumini (hata kama ana baadhi ya madhambi) si kama kafiri hapa duniani na akhera, kama alivyoeleza Imaamu Attwahaawy, na kua hiyo ndio itikadi ya Ahlu Ssunna wal jama'a.

chakushangaza na kusikitisha, ni kuona Abdurrah'maan kupotosha hii sehemu ya pili ya ri'aya (uangalizi) wa Allah kwa waumini!

kwani yeye amewatoa waislamu wafanya madhambi makubwa, kwenye hii ri'aya (uangalizi na msaada) maalumu wa Allah kwa waumini!

na kuwafanya wako sawa na makafiri kwenye

uangalizi wa mwanzo, na hawana uangalizi wowote kutoka kwa Alla unaowatafautisha na makafiri, kama ule unaowatafautisha waislamu waliokamilika imani!

Na kwa hakika hii ni itikadi ya wazi kabisa ya kikhawariji! Na ni takfiri iliowazi kabisa, ambayo anatakikana atubie kwa Allah!

TATU:

Katika muqtadhwa tuliyofafanua hapo, ni vyema kutaja qauli ya Imaam **Ibnu O'thaimiin** Alla amrehemu ambapo ameigawanya walaya katika namna mbili, akasema:

"النوع الأول : عامة ، وهي الشاملة لكل أحد ، قال الله تعالى : (وَرُدُّوا إِلَى اللَّهِ مَوْلاهُمُ الْحَقِّ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ) [يونس : ٣٠] ، فجعل له ولاية على هؤلاء المفترين ، وهذه ولاية عامة .النوع الثاني : خاصة بالمؤمنين ، قال تعالى : { ذلك بأن الله مولى الذين آمنوا وأن الكافرون لا مولى لهم } [محمد : ١١] ، وهذه ولاية خاصة".

القول المفيد على كتاب التوحيد ٣/١٠١-١٠٢. دار العاصمة.

"Na walaya ya Alla iko namna mbili, **namna ya kwanza**:

ni **walaya ya ujumla**, nayo ni ile inayoenea kwa kila mmoja, amesema Alla mtukufu-katika suuratu yuunus, aya ya 30-: "na wanarudishwa kwa

Alla(maulaahum) mola wao wa haki, na vimepotea vile walivyokua wakimzushia uongo Alla vya kumshirikisha katika ibada"

Alla amejaalia kua ana walaya kwa hao waongo, na hii ni walaya ya ujumla(yenye maana ya kuteza nguvu, na kuendesha mambo ya waja, na nk).

Namna ya pili ya walaya:

Ni ile inayo wahusu waumini, amesema Alla mtukufu: "hilo ni kwa sababu Alla ni walii wa walio amini, na makafiri hawana walii"-suurat Muhammad aya 11-,Na huu ni uwalii maalumu(kwa waumini)".

Tazama: Alqaulul mufiid alaa kitaabi Ttauhiid 3/101-102.

Tunaona hapo, Al Imaam Ibnu O'thaimiin, amegawanya walaya ya Alla, ambayo inafanana na ria'ya yake makundi mawili, kwanza inayongia kwa watu wote, waislamu na makafiri, pili inayoingia kwa waislamu tu.

na maneno yake yako wazi kua hii yenye maana maalumu, inaingia waumini wote, kwa ushahidi wa Aya aliyotoa, ambayo inaeleza kuwa: ALla ni Walii wa walio amini, na makafiri hawana walii.

Na ndio maana kwenye tafsiri yake akasema tena:

"والله ولي كُلِّ أحد، وهذه هي الولاية العامة ، أليس الله تعالى يرزق الكافرين وينمي أجسامهم وييسر لهم ما في السموات والأرض، وسخر الشمس والقمر والنجوم والأمطار؟! هذه ولاية، ويتولى المؤمنين أيضاً بذلك؛ لكن هذه ولاية عامة.

أما الولاية الخاصة، فهي للمؤمنين. قال تعالى:) اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ آمَنُوا يُخْرِجُهُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُمْ مِنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ)(البقرة: من الآية٢٥٧)، والولاية الخاصة تستلزم عناية خاصة".

تفسير ابن عثيمن لآية رقم ٢٦ لسورة الكهف.

"Alla ni walii wa kila mtu, na huu ni uwalii wa ujumla (unaoingia waislamu na makafiri), hivi Alla si anawaruzuku makafiri? Na anakuza miili yao? Na anawawepesishia vilivyoko mbinguni na ardhini? Na anaziendesha jua na mwezi na nyota na mvua?

Hii ndio mana ya walaya hii.Na Alla anawasimamia waumini pia kwa walaya hii, lakini hii ni walaya ya ujumla(inayohusu waislamu na wasio waislamu).

Ama walaya maalumu, hii ni maalumu kwa waumini tu, amesema Allah mtukufu:

(Alla ni walii wa wale walio amini, anawatoa kutoka kwenye giza, kuwaingiza kwenye nuru, na wale waliokufuru mawalii wao ni matwaaghuuti, wanawatoa kutoka kwenye nuru, wanawaingiza kwenye giza la ukafiri). Na walaya (hii) maalumu, inalazimika kupatikana

riaya (uangalizi) maalumu"

Tazama: Tafsiri ya Shekh Ibnu O'thaimiin ya aya namba 26 ya suuratul kahfi.

Maneno hayo ya Imaam Ibnu O'thaimiin, yamezidi kuweka wazi makusudio ya walaya maalumu hapa, ambayo si ile ya waumini na makafiri kwa ujumla, bali walaya hii ni ya waumini tu (wote), na haingii kafiri.

Na hakuna shaka kua kwenye walaya na uangalizi huu anaingia kila muumini kwa kadri ya imani yake, na haiwezekani ikawa hakuna tofauti kati ya muislamu mwenye madhambi na kafiri katika uangalizi wa Alla.

Kwani ule uangalizi wa ujumla unaoingia ndani yake makafiri na waislamu ni uangalizi wa kumiliki, na kutoa rizki, na kulea na nk.

Ama uangalizi maalumu kwa waumini maana yake, ni kama alivyosema Al Imaam **Asshinqiitwi kua:**

"وهذه الولاية المختصة بالمؤمنين هي ولاية الثواب والنصر والتوفيق والإعانة".

أضواء البيان ٣/٢٥٧

"Na hii walaya maalumu inayokusudiwa waumini tu(pasi na makafiri), ina maana ya walaya ya kuwapa thawabu, na kuwapa ushindi, na kuwapa taufiq ya kuiendea haki, na kusaidia"

Tazama: Tafsiri ya Shekhe: Adh'waaul bayaan 3/257.

Kwahiyo ikiwa uangalizi huu wa waumini unatofautiana na ule wa wanaoingia ndani yake makafiri kwa kuwapa thawabu, na kuwaongoza katika haki, na msaada na nk: watafanana vipi waislamu wenye madhambi makubwa na makafiri kwenye riaya alioitaja Abdrurrah'maan?

Kwani waislamu wenye madhambi makubwa hawapati thawabu katika yale mema wanayofanya? Je kukubali kwao uislamu na kuamini hakuna taufiq ya Alla katika hilo? Na je hilo haliwatofautishi na makafiri?

Sina shaka ndugu msomaji umeelewa vizuri maudhui hii, na umejua uhakika wa makosa

aliyoingia Abdurrah'maan na Ame katika maswala haya nyeti!

NA KWA KUMALIZIA MAUDHUI HII:

nataka niwape zawadi muhimu kuhusiana na kulitumia neno Hizbu Llaah kwa Waislamu wote, nayo ni maneno ya Assheikh Ibnu O'thaimiin, pamoja na Assheikh Muqbil Alwaadi'i.

Ama shekh Ibnu O'thaimiin amesema:

"لو قال قائل: هل الحزبية مشروعة؟ الجواب: الحزبية بين المسلمين غير مشروعة، بل هي أداة للتفرق، أما الحزبية بين الكفار وبين المسلمين واجبة، لأن غير المسلمين هم حزب الشيطان، فالله تعالى جعل لنفسه حزبا، وجعل للشيطان حزبا، ولا بد من هذا، لكن بين المسلمين محرمة، لأنها تؤدي إلى الفرقة"

.تفسير القرآن لابن عثيمين ٢/٥٩ دار ابن الجوزي

"Lau kama atasema mwenye kusema na kuuliza: hivi umakundi umejuzishwa? Jawabu: umakundi kati ya waislamu ni jambo lisilo la kisheria, bali ni njia ya kufarakanisha.

ama umakundi kati ya makafiri na waislamu ni wajibu, kwa sababu wasiokua waislamu ndio Hizbu Sshaitwaan(kundi la shetani).

Kwa hiyo Alla amejiwekea kundi, na amemfanya shaitwaan kua na kundi, na hili ni lazima, lakini umakundi huo kati ya waislamu(wakawa na mavyama na mapote pote) ni jambo liloharamishwa, kwa sababu linapelekea kwenye kufarikiana"

Tazama: Tafsiri ya Ibnu othaimiin 2/59.

Maneno haya ya sheikh Ibnu O'thaimiin yako wazi hapo, kua Alla mtukufu, amewaita waislamu kwa ujumla kua ni Hizbu Llaah dhidi ya makafiri, ambao ni Hizbu Sshaitwaan.

Na akatanabahisha kua, kati ya waislamu wenyewe kwa wenyewe hawatakikani kua na makundi makundi, na kua wenye kuanzisha makundi makundi katika uislamu, wanatoka katika Hizbu LLaah iliyokamilika na iliosafi, **na ndio maana akasema tena** (Ibnu Othaimiin):

"كل المسلمين حزب لله عز وجل، والدين الإسلامي حزب واحد، ومن خالف خرج عن هذه الحزبية".

تفسير القرآن لابن عثيمين ٢/٥٩ دار ابن الجوزي

"Waislamu wote ni Hizbu ya Alla (ni kundi la Alla), na dini ya kiislamu yote ni kundi (Hizbu) moja, na mwenye

kukhalifu anatako katika hii hizbiyya"

(kwa maana akiingia kwenye ukafiri anatoka moja kwa moja, na akikhalifu kwa kufanya dhambi zisizomtoa kwenye uislamu anatoka kutoka kwenye Hizbu ya Allah iliokamilika na hatoki moja kwa moja kwenye asili ya Hizbu yake)

Angalia tafsiri Ibnu Othaimiin 2/59.

Na amesema tena, alipokua anasisitiza uharamu wa makundi makundi na mavyama ndani ya uislamu:

لأن بني آدم كلهم حزبان: الإيمان والكفر، قال تعالى: (هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُؤْمِنٌ)–سورة التغابن:٢– هذا لا بد منه، لكن أحزاب في الحزب الواحد هذا خلاف الإسلام.".

تفسير ابن عثيمين ٢/٦٠

" Ni kwa kua wanadamu wote ni Hizbu mbili (makundi mawili) Hizbu ya Imani, na Hizbu ya kufru, amesema Allah mtukufu: (yeye Alla ndie aliyekuumbeni, wako miongoni mwenu makafiri, na wako miongoni mwenu waumini).

hili (la kugawanyika kati ya waislamu na makafiri) lazima litokee.Lakini (kuanzisha) makundi katika kundi moja (la Hizbu LLaah) hii ni kinyume na uislamu"

Tazama tafsiri ya Shekhe Ibnu O'thaimiin 2/60

Na hapo tena shekhe ameelezea Hizbu Llaah na Hizbu Sshaitwaan kwa maana ya ujumla, kua Hizbu Llaah ni waislamu, na Hizbu Sshaitwaan ni makafiri.

Na akasisitiza kua kunzisha makundi makundi ndani ya Hizbu moja (yani ndani ya Hizbu Llaah ambao ni waislamu) ni kinyume na uislamu.

Kwa hakika kwa ufafanuzi na qauli hizi za wanachuoni zilizo wazi kabisa, sidhani kua watu hawa hawataelewa kosa walilofanya!

Lakini ili kushibisha zaidi ufafanuzi huo, naomba niweke maneno ya Assheikh **Muqbil Al'waadiy**, Alla amrehemu, aliposema:

" ونرى أن الناس ينقسمون إلى حزبين: حزب الرحمن، وهم الذين تنطبق عليهم أركان الإسلام وأركان الإيمان غير رادين شيئا من شرع الله. وحزب الشيطان، وهم المحاربون لشرع الله".

هذه دعوتنا للشيخ مقبل ص: ١٣ دار الآثار.

"Na tunaona kwamba watu wamegawanyika katika Hizbu mbili (makundi mawili) Hizbu Rrah'maan, nao ni wale ambao zinapatikana kwao nguzo za uislamu, na nguzo za imani, wasio rudisha (wasio pinga) chochote

katika sheria za Allah.

Na Hizbu Sshaitwaan, nao ni wale wanao piga vita sheria za Alla"

Tazama kitabu: haadhihii da'watunaa cha Shekh Muqbil uk: 13.

Sina shaka kua maneno hayo ya A'llaama Muqbil yako wazi sana, na hayahitaji sherehe kubwa, kwani amebainisha kua watu wako makundi mawili.

Kundi la Alla, ambalo ni waislamu, na kundi la shaitwaan, nalo ni la makafiri, kwani makafiri ndio wanaopiga vita sheria za Allah.

Lakini pia si vibaya tukawazawadia na hii ya mwisho ya Assheikh **Ab'bul aziiz Arraajihy**, aliposema:

كل المؤمنين حزب واحد، والكفار حزب، المؤمنون حزب، والكفار حزب، المؤمنون حزب الله، والكفار حزب الشيطان".

موقع الشيخ.

"Waumini wote ni Hizbu moja, na makafiri ni Hizbu moja, waumini ni Hizbu na makafiri ni hizbu, waumini ni Hizbu LLaah, na makafiri ni Hizbu Sshaitwaan"

Tazama kwenye websit ya shekhe Abdul Aziiz Arraajihy.

Kwa hakika ufafanuzi huu uko wazi na umeeleweka, na hakuna atakayedhani hajaelewa isipokua amefanya kusudi!

Na ni wito wangu kwa Abdurrah'man na mwenzake wazirejee nafsi zao, na waelewe kua walifanya pupa kukosoa jambo na kujiaminisha walichoongea bila kurejea kwenye vitabu vya wanachuoni!

Endelea kufuatilia makala NAMBA SABA ujionee mengi zaidi katika baadhi ya makosa yao ya kielimu Inshaa Allah.

IMEANDIKWA NA:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM

وفقه الله وغفر له ولوالديه ولجميع المسلمين

١٤٣٨/٤/١٩هـ